JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

## KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

www.kazi.go.tz

Toleo la 7 | Agosti, 2022



# MKATABA HALI BORA

1 Waziri Ndalichako ahamasisha Waajiri kuwa na Mkataba wa Hali Bora kwenye Maeneo ya Kazi.




## WAAJIRI WATAKIWA KUWA NA MKATABA WA HALI BORA KWENYE MAENEO YA KAZI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Prof. Joyce Ndalichako amewataka waajiri nchini kuhakikisha wanakuwa na mikataba ya hali bora katika maeneo yao ya kazi ili kuongeza tija, kuepusha migogoro na kudumisha mahusiano mema.

Amesema hayo Agosti 26, 2022 katika hafla ya uwekaji saini Mkataba wa Hiari wa Hali Bora kati ya Menejimenti ya Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC), na Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) Tawi la Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC).

Ameeleza kuwa, Makubaliano ya Mkataba wa Hali bora ni hatua ya utekelezaji wa Sheria za kazi hususani Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 ambayo uweka mazingira wezeshi ya kisera, kisheria na kitaasisi baina Wafanyakazi na Waajiri kwa lengo la kuboresha mazingira bora ya kazi, maslahi ya Wafanyakazi na kuleta tija mahala pa kazi.

“Ninafarijika kushuhudia waajiri kama kampuni ya TCC mnavyowajali wafanyakazi kwa kuchukua hatua hii ya kuwa na mkataba wa hali bora, ni kielelezo tosha mmedhamiria kuboresha maslahi ya Wafanyakazi na kuongeza hali ya kazi na uzalishaji,”

Aidha, Waziri Ndalichako ametoa rai kwa Waajiri kufunga mikataba ya hali bora na wafanyakazi ili waweze kuboresha maslahi ya Wafanyakazi wao, kuongeza tija, uzalishaji na kuweka bayana malengo na wajibu wa Wafanyakazi na mwajiri.

Sambamba na hayo Mhe. Ndalichako alieleza kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali vyama vya waajiri na wafanyakazi pamoja na shirika la Kazi Duniani (ILO) wapo kwenye mchakato wa kukamilisha rasimu ya sera ya Taifa Ajira (2008), lengo ni kukuza fursa za ajira na kazi za staha ili kupunguza ukosefu wa ajira, umaskini na hatimaye kuongeza tija na uzalishaji kama inavyoainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025.



# KIWANDA CHA CHAI MPONDE CHA KAMILIKA 95%

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), Mhe. Profesa Joyce Ndalichako ametembelea kiwanda cha Chai Mponde kilichoko Bumbuli, Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga na kuwahakikishia wakulima wa zao hilo kwamba kiwanda kimekamilika kwa asilimia 95%.

Mhe. Profesa Ndalichako ameyasema hayo Agosti 16, 2022, ikiwa ni siku sita tu baada ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Comrade Daniel Chongolo kutoa maelekezo, juu ya kiwanda hicho kwamba kitakapoanza uzalishaji wa majaribio Septemba mwaka huu, kiendelee kupokea na kuchakata Chai moja kwa moja.

Pofesa Ndalichako amesema "Kimsingi kiwanda kimekamilika kwa asilimia 95%, nimefanya ukaguzi kwenye eneo la kupokelea na kuchambua Chai, eneo la kuichakata (Processing), eneo la kuangalia viwango na ubora (Grading), eneo la Karakana, Tanuri la kufua joto (Boiler) na kote huko kumekamilika."

Baada ya kupokea maelekezo Waziri alisema wao kama Wizara alikaa na Katibu Mkuu pamoja na Watendaji Wakuu wa Mifuko ya Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ambao ndio wawekezaji wakuu kwenye kiwanda hicho ili kuona namna bora ya kuanza utekelezaji mara moja.

"Kulikuwa na baadhi ya vifaa ikiwemo mabomba ya kutolea mvuke na nyavu za kukaushia chai ambavyo vilihitajika ili kukamilisha hatua za uzalishaji." alifafanua.

Alisema Kiwannda cha Chai Mponde kinakwenda kuwa kiwanda cha ksiasa na kitakuwa na uwezo wa kuchakata tani 5,800 na baadaye uzalishaji utafika tani elfu 16,000.

"Kwa siku wakulima watauza kilo elfu 52,000, naamini kwamba kiwanda kitaenda kuinyanyua Halmashauri yetu ya Bumbuli na kuboresha maisha ya wananchi." Alisema.

# KATAMBI APONGEZA MIKATABA YA UTENDAJI KAZI

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu Mhe. Patrobas Katambi amepongeza Mfumo wa kuingia Mikataba ya Utendaji Kazi na Taasisi za Umma ambao unaainisha malengo yatakayo tekelezwa na Taasisi za Umma katika kipindi cha mwaka mmoja.

Ameyasema hayo hii leo Agosti 14, 2022 Jijini Arusha wakati wa kikao kazi cha menejimenti ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu cha kufanya tathmini ya utendaji kazi wa kwa mwaka 2021/22 na kuweka malengo, na kusaini mikataba ya Utendaji Kazi kwa Mwaka 2022/23.

"Mfumo huu una faida nyingi ikiwa ni pamoja na kuongeza uwajibikaji katika utekelezaji wa Sera, Mikakati na vipaumbele vya Taasisi za umma na vya kitaifa"

Pamoja na hayo Mhe. Katambi ameisisitiza menejimenti ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kufanya kazi kwa bidii na kuwa wabunifu katika maeneo yao ya kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika kazi tunazozifanya.

Aidha, amehimiza mshikamano na kufanya kazi kama timu kwa kuwa, Ofisi hiyo ndiyo Kioo na Kiongozi kwa Wizara nyingine, hivyo amewataka kuweka usimamizi madhubuti katika Programu, Miradi na kazi zote ambazo zinasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Kwa upande wake Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu Prof. Jamal Katundu ameeleza kuwa mikataba hiyo ya utendaji kazi itasaidia ofisi hiyo na taasisi zilizopo chini yake kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kutekeleza kwa ufanisi maelekezo wanayopatiwa na Viongozi na hatimaye kuleta maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara hiyo ikiwemo Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) walishiriki katika kikao kazi hicho.






## MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2022 ZAFANIKISHA FEDHA ZA MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA KUREJESHWA

Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2022 zimefanikisha kuzihimiza Halmashauri ambazo hadi sasa zimeukimbiza mwenge huo, kurejesha shilingi Milioni 847.6 katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Fedha hizo hutolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu -Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kupitia Halmashauri kwa ajili ya mikopo yenye riba nafuu kwa Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu -Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu Mhe. Patrobas Katambi ameyasema hayo, leo Agosti 16, 2022 wakati wa makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kutoka uongozi wa mkoa wa Singida kwa mkoa wa Dodoma, wilayani Bahi.

Mhe. Katambi amefafanua kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan imeweka mipango Madhubuti ya kuweza kuhakikisha vijana wanashiriki katika shughuli za kiuchumi.

Amesisitiza kuwa katika kutimiza dhamira ya Mhe.Rais Samia, wakimbiza mwenge wa uhuru kwa mwaka 2022 wamekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa ili wanufauka wengi wapate mikopo.

“Mwenge ni jicho katika kuhakikisha maendeleo yanakuwepo. Majukumu yasipotekelezwa, uzembe, ubadhilifu ukifanyika lazima uchukue hatua, hivyo ni vyema kila mmoja akawe makini katika eneo lake la kazi”

Inaendelea Uk. 6

Mhe. Katambi amebainisha kuwa, hadi kufikia Agosti 14 mwaka huu, Mwenge wa Uhuru tayari umeshatembelea jumla ya Halmashauri 135 kati ya 195 zilizopangwa.

Aidha, ameeleza kuwa mwenge huo umefanikiwa kukagua na kuweka mawe ya msingi katika miradi 941 yenye thamani ya Sh bilioni 551.7.

"Kwa Sasa tayari miradi 64 yenye thamani ya Sh. Bilioni 12.5 imebainika kuwa na dosari za kukosa nyaraka na changamoto za kiufundi"

Kwa upande wake, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa Kwa mwaka 2022, Sahil Gelaruma, amesema mikopo yenye riba nafuu kwa vijana, katika mkoa wa Dodoma ya Sh. Milioni 150 haijarejeshwa Serikali Kuu.

"Mwenge wa Uhuru unaagiza halmashauri hizo kurejesha Fedha hizo haraka kabla mwenge wa uhuru haujapita katika halmashauri zao"





# BORESHENI MAZINGIRA YA KAZI KIAFYA - KATAMBI

Na: Mwandishi Wetu - **Mbeya**

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Patrobas Katambi ameuagiza uongozi wa Kiwanda cha Mbeya Cement kuhakikisha unatafuta mitambo ya kisasa kwa ajili ya kudhibiti vumbi la saruji inayozalishwa kiwandani hapo.

Mhe. Naibu Waziri Katambi ametoa agizo hilo Agosti 26, 2022 alipofanya ziara ya kushtukiza ya kukagua kiwanda hicho na kufuatilia utekelezaji wa sheria za kazi na masuala ya Usalama na Afya mahala pa kazi.

''Sijaridhishwa na hali niliyoikuta kimsingi eneo la uzalisha kuna vumbi ambalo limeshindwa kudhibitiwa na hivyo watumishi kuwa katika hatari kubwa ya kuugua magonjwa"

Mhe. Katambi alisisitiza kuwa usalama wa watu kazini ni muhimu na serikali itaendelea kusimamia sheria ili Watanzania wafanye kazi katika hali ya usalama sehemu za kazi.

"Katika kipindi cha mwezi mmoja nahitaji kuona mabadiliko ya namna ya kudhibiti vumbi ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa vifaa vya kujikinga na vumbi (barakoa)."

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mbeya Cement, Khaledi Ghaleib alisema watahakikisha wanatekeleza maagizo hayo ya kuthibiti mifumo ya kusambaza kwa vumbi na kuwepo kwa vifaa vya kujikinga kwenye eneo la uzalishaji.





# TANZANIA NA QATAR ZAJADILI AJIRA WAKATI WA KOMBE LA DUNIA

Tanzania imeihakikishia Qatar kuwa ipo tayari kutoa vijana watakaoweza kufanya kazi nchini humo, hususan katika kipindi hiki ambacho mahitaji ya nguvukazi ni makubwa kutokana na nchi hiyo kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu wa Kombe la Dunia yatakayochezwa mwezi Novemba 2022.

Ujumbe wa Tanzania ulioongozwa na Katibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Jamal Katundu, umebainisha hayo wakati wa kushiriki mazungumzo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Qatar, Dkt. Ahmad Hassan Al-Hamadi kwenye Ofisi za Wizara hiyo Jijini Doha, Qatar tarehe 28 Agosti 2022.

Mazungumzo hayo yamefanyika ikiwa ni moja ya utekelezaji wa Mkataba wa Kazi uliosainiwa kati ya Tanzania na Qatar mwaka 2014.

Ujumbe huo umeipongeza Qatar kuwa mwenyeji wa Kombe la Dunia la FIFA litakaloanza mwezi Novemba mwaka huu.

Aidha, Umewafahamishwa kuwa Tanzania imewaandaa vijana wake wenye ujuzi na hivyo kuombwa kupata nafasi za ajira na za viza (visa allocation) kwa ajili ya Watanzania kuweza kuja kufanya kazi Qatar hasa wakati wa kombe la Dunia.

Katika Kikao hicho, viongozi hao pia wamesisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano mzuri uliopo kati ya nchi hizi mbili hususan katika maeneo ya uwekezaji na biashara.

Viongozi hao wamefafanua kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imefanya maboresho makubwa ya mazingira ya uwekezaji na biashara, hivyo wametoa wito kwa wafanyabiashara wa Qatar kuja kuwekeza nchini katika maeneo kama vile utalii, kilimo, madini, maliasili, uvuvi na utamaduni.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Prof. Joyce Ndalichako akishiriki zoezi la ugawaji vifaa wezeshi kwa Watu wenye Ulemavu lililoandaliwa na Shirika la kutoa misaada la Shree Lohana Mahajan na Lal Baug Pariwar.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Patrobas Katambi akizungumza na Wafanyakazi wa alipofanya ziara ya kushtukiza katika Kiwanda cha Mbeya Cement kwa lengo la kukagua utekelezaji wa Sheria za Kazi na masuala ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi .





Ujumbe wa Serikali ya Tanzania ukiongozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Prof. Jamal Katundu (wa tatu kutoka kushoto) walipokutana na kufanya mazungumzo na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kazi Qatar, Mohammed Hassan Al - Obaidly Jijini Doha Agosti 29, 2022.

KATIBU MKUU
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**
S.L.P 2890
**DODOMA, Tanzania**
Barua pepe: ps@kazi.go.tz
**www.kazi.go.tz**
@Ofisi ya Waziri Mkuu_Kazi